# REPUBLIC OF KENYA

## COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

### THE HANSARD

**Thursday, 31st August, 2023**

*The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.*

*[The Speaker (Hon. Lantano. Nabaala) in the Chair]*

PRAYERS

**QUORUM CALL**

**Speaker:** Clerk, confirm whether we have got quorum.

*(Lack of quorum confirmed)*

**Speaker:** Without quorum, I direct that the bell be rang for ten minutes.

*(Quorum bell rung for ten minutes)*

**Speaker:** Clerk, confirm whether we have got quorum.

*(Clerk confirmed achievement of Quorum)*

**Speaker:** Now that we have got quorum, let the bell stop ringing.

**NOTICE OF MOTION**

EL NINO PREPAREDNESS

**Hon. Stephen Ndiritu:** Thank you, Hon. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT AWARE THAT, part two Firefighting services and disaster management is a function of the County Government as stipulated in the Constitution of Kenya, 2010;

AWARE THAT, according to Ministry of Environment, Natural Resources & Regional Authorities, Kenya Meteorological Department has issued a press release that most parts of the country, Laikipia County included are likely to receive El Nino rains between the Months of October, November and December 2023;

FURTHER AWARE THAT, the implication of above rains during the season is floods and flash floods (urban floods), enhanced water levels in the rivers, problems related to water borne diseases are likely to occur due to the expected heavy rains;

CONCERNED THAT, Water borne diseases and vectors are expected to increase leading to possible upsurge of diseases like malaria, dengue fever, schistosomiasis, typhoid, cholera, Rift Valley Fever (RFV), and lymphatic filariasis;

FURTHER CONCERNED THAT, the expected enhanced rainfall is likely to lead to muddy and slippery conditions on the roads in most parts of the County.

This House URGES the County Government;

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

1. To do re-afforestation by planting trees in areas where forests and environment has been degraded as there are better chances of these trees establishing during this coming season.
2. To urgently construct storm drainage systems and open up clogged ones to avoid urban flooding in towns from surface runoff triggered by heavy rainfall storms.
3. The department in charge of Environment, Water and Natural Resources to lay down strategies of mitigating any negative impacts that will be associated with these heavy rains.
4. The department of Health should, pre-position relevant medical supplies in all health facilities to be able to deal with waterborne diseases.
5. The above department to adjust their individual budgets to meet intervention measures in case of the rains.
6. Employ dedicated street cleaning crews to regularly sweep and clean public spaces.

**MOTION**

EL NINO PREPAREDNESS

**Hon. Stephen Ndiritu:** Thank you, Hon. Speaker. I beg to move the following motion;

THAT AWARE THAT, part two Firefighting services and disaster management is a function of the County Government as stipulated in the Constitution of Kenya, 2010;

AWARE THAT, according to Ministry of Environment, Natural Resources & Regional Authorities, Kenya Meteorological Department has issued a press release that most parts of the country, Laikipia County included are likely to receive El Nino rains between the Months of October, November and December 2023;

FURTHER AWARE THAT, the implication of above rains during the season is floods and flash floods (urban floods), enhanced water levels in the rivers, problems related to water borne diseases are likely to occur due to the expected heavy rains;

CONCERNED THAT, Water borne diseases and vectors are expected to increase leading to possible upsurge of diseases like malaria, dengue fever, schistosomiasis, typhoid, cholera, Rift Valley Fever (RFV), and lymphatic filariasis;

FURTHER CONCERNED THAT, the expected enhanced rainfall is likely to lead to muddy and slippery conditions on the roads in most parts of the County.

This house URGES the County Government;

1. To do re-afforestation by planting trees in areas where forests and environment has been degraded as there are better chances of these trees establishing during this coming season.
2. To urgently construct storm drainage systems and open up clogged ones to avoid urban flooding in towns from surface runoff triggered by heavy rainfall storms.
3. The department in charge of Environment, Water and Natural Resources to lay down strategies of mitigating any negative impacts that will be associated with these heavy rains.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

4. The department of Health should, pre-position relevant medical supplies in all health facilities to be able to deal with waterborne diseases.
5. The above department to adjust their individual budgets to meet intervention measures in case of the rains.
6. Employ dedicated street cleaning crews to regularly sweep and clean public spaces.

Bwana Spika, huu ni mswada ambao nimeonelea ni vizuri niulete kwa sababu tuko na onyo ambazo tumepewa kutoka idara ya hali ya anga ya kwamba huenda kukawa na mvua kubwa ya El-nino. Kama hii mvua itaweza kufika na tuwe hatujajitayarisha, huenda tukapatwa na madhara ambayo tutashindwa kuzuia,

Kwa hivyo Bwana Spika, ni vizuri kuhakikisha ya kwamba yale mambo ambayo yanafaa kufanywa imefanywa mapema. Ni vizuri pia kuweza kuelezea wananchi huko mashinani ambao ni wafugaji na wakulima waweze kutayarisha mashamba yao kwa sababu mvua itakaponyesha, itakuwa ni jambo la aibu kama itanyesha na kuisha na tubaki na njaa. La pili, itakuwa ni aibu na zile bwawa ambazo tuko nazo serikali haitaweza kuchukua nafasi hii ya mwezi mmoja kuzichimba ili tupate maji ya kutosha na tuweze kujiwekea ingine.

Lingine ni kuhusu magonjwa ambayo hupatikana wakati kunaponyesha mvua nyingi kama vile nimeyataja katika huu mswada. Ni vizuri serikali kupitia Idara ya Afya iweze kuhakikisha ya kwamba tumeweza kupata dawa katika zahanati ambazo zimekaribia wananchi. Kwa hivyo, huu ni mswada ambao ni wa kufahamisha serikali kwa sababu huenda wakasahau au kupuuzilia inavyosemekana kuhusu El-nino.

Kama Wajumbe, ni jukumu letu kuwakumbusha na kuwaeleza ya kwamba sisi tuko macho na lolote ambalo litakapofanyika kwa njia mbaya na serikali ingeweza kuzuia, basi tutakuwa chonjo na wale ambao watapatikana kwa kona mbaya, tunaweza kuwachukulia hatua kama kuachishwa kazi kama shida inaweza kutokea na tayari ilikuwa imetangazwa. Ni vizuri wakati mtu yuko na kazi ambayo iko mbele yake ili kila wakati uwe chonjo. Sasa hivi mimi niko chonjo. Leo hii nimenunua mahindi na kutoka kesho kuendelea nitapanda. Kwa hivyo mimi tayari najitayarisha na ni vizuri pia nao wananchi wajitayarishe. Wale ambao wanafanya kazi katika serikali ni lazima wajitayarishe kukinga wananchi.

Haya ni mambo ambayo naonelea ni vyema kuyaleta hapa ili huu mswada upite na hivyo, tutaweza kusaidia serikali na wananchi ambao wametupatia hii nafasi. Kuna mambo mengi ambayo nimetaja Bwana Spika lakini najua ya kwamba Wajumbe wamepitia huu mswada na pia utaweza kupelekwa ule upande mwingine wa serikali, nafikiria itakuwa ni jambo la busara kuhakikisha ya kwamba tumeuangalia ili tuweze kupitisha. Kwa hayo machache, ninamuomba Naibu wa Spika, Mheshimiwa Anthony Wambui aweze kuafiki huu mswada. Asante.

**Hon. Anthony Theuri:** Asante sana, Bwana Spika kwa hii nafasi na pia kwa Mheshimiwa Ndiritu kwa kuniamini ya kwamba nitaafiki huu mjadala. Ni kweli yale yote imesemwa na inastahili tujitayarishe. Mzungu alisema ya kwamba wakati haujajitayarisha, unajitayarisha kuanguka. Haya mambo ameongea kama nabii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hapa nje, sasa hivi unaona mawingu ambayo ni ya mvua. Serikali yetu Kuu ya Kenya imeweka pesa nyingi katika Idara ya Hali ya Anga ili kuhakikisha ya kwamba Wakenya tunajulishwa kila wakati. Wakati wa jua, sisi huambiwa ya kwamba jua inakuja. Wakati huu wametuambia ya kwamba mvua inakuja. Mheshimiwa Spika, sisi tunastahili kuwa kipao mbele. Haya maji ambayo yanakuja, El-nino haitaishi milele na baada ya siku chache tu tuanze kulia hatuna maji.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Bwana Spika, sasa hivi, hawa Waheshimiwa watakuambia ya kwamba wameanza kupata shida ya maji kila mahali. Kuhusu mvua inayokuja, kama hatutachukua nafasi kama serikali ama kibinafsi ya kuhifadhi hiyo maji au kulima, tutarudi hapa na kuanza kufanya bajeti ya ziada ya kwamba watu wetu wako na njaa na pia kuwanunulia maji, ilhali Mungu ametupatia nafasi nzuri ya kutumia hii El-nino. Maisha huangaliwa na ule mtazamio ambao uko mbele yako.

Usiangalie lile jambo ambalo liko mbele yako kama jambo ambalo linakuja kukumaliza. Kama ni jua, unachukua nafasi hiyo. Wakati wa jua kama ulikuwa umelima kama Mheshimiwa Kanyutu au Mheshimiwa Kuria ambao walikuwa wamelima mboga, wanatuuzia kwa bei uliyo juu ili na kupata pesa yako. Jua haitakuja kutumaliza kama tutaitumia vizuri. Vile vile kupitia hii mvua tupande na tusaidie wananchi wetu. Idara ya Afya na Mazingira pia iweze kuenda Likii, soko na kwingineko wakinyoosha mitaro mapema. Tuambie watu walioko kwa mito pia waweze kutoka kwa sababu mvua inakuja.

Tupate kuangalia njia zote ili tuweze kukinga na tusije hapa kulia baadaye. Nikimaliza, Biblia inasema, ni nani huyo ambaye hawezi kukaa chini afanye hesabu ya mjengo wake, nani huyo mjinga mbaye atajenga mjengo wake juu ya changa. Tuwe werevu na wajanja na tuache kulia kila wakati ilhali tumebarikiwa sana. Hakuna nchi ambayo imebarikiwa kama Kenya kwa sababu kuna misimu wa jua na pia mvua. Sisi tuka pahali ambazo tumeelekezwa kabisa. Tuwache ufisadi na ujinga wa kujitakia. Tuhakikishe ya kwamba hii mvua itakuwa ya baraka na tusilete siasa ndogo ndogo.

Kama wewe umeambiwa na Mheshimiwa Ndiritu watu wako waondoke kwa mitaro, basi waondoke kwa sababu sisi hatutaki kuzika watu. Kama ni Mheshimiwa wa Igwamiti (001) aweze kupanga watu wake wa Manguo na sokoni sawa sawa ili mambo ipangwe. Kama tutatumia mvua ambayo inakuja vizuri, basi italeta baraka kwetu. Ole wetu kama hatutasikiliza Mheshimiwa Ndiritu. Tutakuja kumuita nabii wa ukweli kwa sababu ametoa unabii wake na sisi kama Wabunge ni kusikiliza ili tujiulize kama tutafuata huo unabii. Kwa hayo machache, naomba wenzangu tupitishe huu mjadala hata bila kuongea. Muamini Kagondu, mimi na hadi Spika wetu ili tumalize hayo maneno na tuweze kuelekea kwa biashara nyingine.

*(Question proposed)*

**Hon. Salim Edung:** Asante, Bwana Spika kwa kunipa hii nafasi. Siku ya leo ni siku muhimu sana kwa sababu Mheshimiwa Kagondu ameleta mswada ambao watu wengi walikuwa wanatarajia kuangalia kwa makini sana. Wakati tulipata taarifa tulisikia ya kwamba katika hizo miezi mitatu ambazo zimetajwa kuna mvua kubwa itakayonyesha katika nchi hii yetu. Ukirejelea kwenye Biblia, wakati wa Nuhu watu walielezwa wajenge safina kwa sababu mvua kubwa inanyesha, bali watu wengi walipuuza. Wenye walipuuza walipata shida ambayo walipata.

Kwa sababu sisi tumepata habari tukiwa Waheshimiwa kwenye Bunge hili, inafaa twende makanisani tuwaeleze watu wetu ya kwamba kuna mvua inakuja, tuweke mipangilio. Hasa ukiangalia sisi wafugaji tunapenda kujenga kwenye laga kwa sababu tunajua hapo ni mahali pazuri palipo na mteremko, lakini sasa tutaenda kuwaambia watu wetu ya kwamba kuna mvua inayokuja na ni kubwa sana. Inafaa twende juu mlimani na tusikae karibu na mito, kwa sababu kuna mito mikubwa na mito midogo inayoitwa laga.

Vilevile, mswada huu ambao umeletwa na Mheshimiwa Kagondu umekuja kwa njia inayostahili. Ukiangalia hizo miezi ambazo zimetajwa pale na sasa tunaelekea Mwezi wa Tisa, inaonyesha ya kwamba sisi tukipeana habari huko makanisani, barazani, na pia waalimu wapeane shuleni tutakuwa tumezingatia kile Wanasayansi wanachosema. Mwanasayansi

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

akitaja kitu wakati mwingine, wananchi wanalichukua kama uongo bali athari huja baadaye. Inafaa pia tujipange katika hospitali zetu kwa sababu tunajua ya kwamba ugonjwa wa kipindupindu utakuja wakati wa hii mvua kwa sababu mafuriko yatakuwa kila mahali. Tunastahili kutahadhari kwa sababu ya jambo kama hilo.

Kwa upande wa maji, inastahili tuweke mikakati ya kuweka mabwawa mengi ili tupate maji. Wakati tutajenga hayo mabwawa tutapata maji ya kufanya unyunyuziaji wa maji shambani mvua itakapoisha. Ninaunga mkono huu mswada na kuomba Wabunge wenzangu pia waunge mkono kwa sababu itatusaidia sisi pamoja na wananchi wa nchi yetu ya Kenya. Asante.

**Hon. Simon Kanyutu:** Thank you, Mr. Speaker. I stand to support the motion from the Hon. Member but I am concerned because it is as if the Hon. Mover was seated somewhere with yesterday's Mover of the motion on waste and refuse management. With the terms that he has used here such as schistosomiasis, the last time I heard that word was in secondary school. The other one is lymphatic filariasis which I remember very well is caused by parasites during the rainy season. I appreciate his move, and this motion is one of the best. My concern was if they had sat together with the person who moved yesterday's motion. It is a very remarkable motion in which they are catering for our people. They are concerned on how the future of our people will be if they are not getting proper information for preparedness. So, I thank the Mover and wholly support. Thank you.

**Hon. Irene Wachuka:** Asante sana, Mheshimiwa Spika. Kwanza nataka kumshukuru Mheshimiwa Ndiritu kutoka kwenye Wadi ya Thingithu ambaye ameleta mjadala muhimu sana. Sasa ni wakati wetu na kila mtu anasikia kwenye kila pembe ya Kenya, redio na Runinga zikitangaza kwamba El Nino yaja. Tusipojipanga, tutapangwa na magonjwa kama kipindupindu na homa ya tumbo. Nikikumbuka mwaka wa 2007 ama 2006 katika makaazi ya Maina kulikuwa na ugonjwa na maombolezi kwenye kila pembe kutokana na homa ya matumbo. Kama tu sasa, tulikuwa tunatangaziwa katika kila pembe kwamba watu wajipange, El Nino yaja, waliojenga karibu na mito waondoke. Sisi hatukusikia. Wakati El Nino inakuja inafagia ugonjwa kutoka mbali sana hata tanzania na kuingia pembe zote za Kenya.

Kwa hivyo ni wakati wetu wa kutayarisha watu wetu na kusaidiana na serikali ili haspitali zetu zipate madawa, kwa sababu najua ugonjwa utakuwa kwenye pembe. Tusipojitayarisha tutatayarishwa na ugonjwa. Nataka kusema asante sana kwa Mheshimiwa Ndiritu ambaye ameleta mjadala muhimu sana.

Hiki sio kitu cha mzaha, kinafaa kishughulikiwe hata na serikali ya Kaunti. Namshukuru pia Mwenyekiti wa Kamati ya Ukulima ambaye yuko hapa. Washirikiane na Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ili kama Bunge tushikane pamoja kwa sababu ugonjwa utakapokuja hautabagua kabila ama kamati. Ugonjwa ukija basi umekuja, na El Nino haina mchezo. Kwa hivyo, mimi naunga mkono na kuomba Wajumbe wenzangu tuzingatie haya mambo.

Pia tumkute Gavana ili aambiwe aanze kujitayarisha. Tutaendelea kuchukua maneno kwamba kuna El Nino mara hakuna. Ukweli ni kwamba El Nino inakuja na inamaliza watu, Ugonjwa pia unawamaliza watu. Maji inabebea watu na magari na kupelekwa mpaka Mombasa.

Hili ni jambo muhimu ambalo si la kuchukuliwa mzaha. Namshukuru Mheshimiwa Ndiritu kwa huu mjadala. Naomba Wajumbe wenzangu waunge huu mjadala mkono. Mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia. Asante sana, Mheshimiwa Spika.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

**Hon. Benson Kuria:** Asante sana, Mheshimiwa Spika kwa sababu ya hii nafasi ambayo umeweza kunikabidhi nikijua kwamba leo ni Alhamisi. Bwana Spika, nashukuru Mola kwa sababu ya hii nafasi. Nikisoma Bibilia katika Matendo ya Mitume tisa, aya ya thelathini na sita, kuna mambo Dorcas alikuwa anatenda katika Kijiji chao. Sisi Waheshimiwa kuna maswala ambayo tutaweza kuja nyumaye kuulizwa ni nini ulifanya wakati ulikuwa mahali pale.

Inasemekana ya kwamba Dorcas alifufuliwa kwa sababu ya matendo ambayo alikuwa ametendea wajane. Mheshimiwa Spika, ningependa Waheshimiwa wenzangu waweze kutafakari na kujua nimesema nini. Kwa sababu ya mjadala ambao tumeweza kuletewa na Mjeledi Mkuu wa Bunge hili (Chief Whip), naona ametoka na angeweza kusikia nikinena kuhusu yale ambayo ameweza kutufikishia jioni ya leo.

Bwana Spika, ameleta mjadala ambao sikuwa nao kwa sababu nikiingia katika Bunge, sikuwa na hilo wazo. Wakati nimeingia katika Bunge, Mjeledi Mkuu wa Bunge hili, Mheshimiwa Ndiritu ameweza kusema jambo ambalo litakuwa msaada mkuu katika Jimbo letu la Laikipia. Mheshimiwa Spika, kuna *subsidy* katika Taifa letu. Maswala makuu ni kupigana na janga la njaa ambayo ni kupunguza bei ya mbolea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nikimuunga mkono najua ya kwamba kwa sababu ametaja mwezi wa kumi kutakuwa na mafuriko makuu, Mjeledi Mkuu ndiye kijiti kikuu ambacho anaweza kuangusha kama vile Musa aligonga alipoambiwa na Mungu *"enenda ongelesha jiwe".* Kuliko kuongelesha, akagonga jiwe maji ikawa kali.

Kwa sababu amenyoosha kidole chake, ametueleza ya kwamba kuna mambo ya tahadhari ambayo yako mbele yetu. Nikimuunga mkono, wakati umefika Waheshimiwa ambao wanawakilisha Bunge la Laikipia waweze kufikishia wananchi wa Laikipia ambao ni zaidi ya milioni moja vile watakuwa na tahadhari ya kuwa kuna janga la mvua. Kuna mafuriko makubwa yanakuja katika Jamhuri ya Kenya na sanasana Jimbo la Laikipia.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kwa sababu kuna tahadhari lakini kama wananchi wa Jimbo la Laikipia watakuwa wamepata mbolea kila mahali, najua wafugaji watabahatika kwa sababu ya mvua. Nyasi itakuwa mingi na wakulima watakuwa wamefaidika kwa sababu mvua itakuwa tele na watakuwa na mbolea ambayo imeteremshwa bei. Hii ni kumaanisha ya kwamba tukifika mwezi wa pili, maisha yatakuwa sawa kwa mwananchi wa Jimbo la Laikipia.

Nikiunga mkono, najua ya kwamba kuna kitu Mwenyezi Mungu ameongelesha Mjeledi Mkuu wa Bunge hili. Kwa sababu ameongea ili nasi tuongee na tuseme, ninamuunga mkono nikijua ya kwamba kuna mahali anatuelekeza. Ninajua tukiunga mkono huu mswada ambao umeletwa na Mheshimiwa Ndiritu, kuna mambo mazuri ambayo yatabadilika katika jimbo letu la Laikipia.

Naunga mkono nikijua kwamba naelekea nyumbani na nitafika salama. Wewe pia ukienda nyumbani utafika salama. Tunakuheshimu na tunakupenda. Napenda Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya kujitokeza kwa wingi. Nikiangalia wiki hii tangu wakati tulikula kiapo katika Bunge hili, sijawahi kuona wingi wa Wabunge katika Bunge kama vile nimeweza kushuhudia juma hili ambalo limepita.

Nikiangalia Jumanne wakati niliingia hapa, tulikuwa na zaidi ya Wabunge kumi na nane. Jana asubuhi tulikuwa na zaidi ya Wabunge ishirini. Jana jioni tulikuwa na zaidi ya Wabunge kumi na tisa. Hili ni jambo la kuonyesha ya kwamba Mwenyezi Mungu anatulinda na kutuongoza katika roho mtakatifu. Wacha tuendelee vizuri ili Bunge letu liweze kuleta

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

mabadiliko ukiwa unaongozwa na roho wa Mungu. Mbarikiwe sana na ninaunga mkono mswada ambao umeletwa na Mjeledi Mkuu wa Bunge hili letu. Asante.

**Hon. Joseph Gitahi:** Thank you, Hon. Speaker. Once some of the seniors speak, like Hon. Irene Wachuka, I don't have to say much. Mine is only to register support of the motion and to understand that although the El Nino rains have adverse effects, they also have positive effects. The huge levels of rainfall that we are about to receive, if we take the actions that we have spoken today, we add more water harvesting activities as anticipatory actions as we wait for that natural occurrence.

Secondly, I want to emphasize what Hon. Salim has said. Information is very important. Therefore, let us go and make our people aware of the same so that we do not have cases where flooding will leave many people homeless and destruction of lives and property.

In Githiga Ward we have got areas that flood and I have taken it upon myself to use all the local media stations that are there to ensure that these people are able to prepare themselves before the El Nino rains start. I don't want to say most of the things that have been said, just to say that the motion is timely and we welcome it. I urge the Members of this House to support the motion. Thank you.

**Speaker:** Thank you, Hon. Gitahi. Seeing the mood of the House, I think it is a critical motion and very timely. I love the way Hon. Ndiritu has raised the matter for this House. I wish to take this opportunity to invite the mover to reply.

**Hon. Anthony Theuri:** Asante sana, Bwana Spika. Nasikia hizi vipasa sauti zikiwa tofauti sana kuliko za mbeleni. Nashukuru wajumbe wenzangu kwa vile wamechangia huo mjadala vizuri. Kuna msemo kwa kimombo ambao husema, *'it is easier said than done.'* Tukitoka hapa, hayo mambo yote ambayo tumejadili, tumesema ya kwamba tutaenda kupanda, tutaongea na watu wetu, tutahakikisha ya kwamba mitaro imesafishwa na tutahakikisha ya kwamba tumejenga vizuri na pia kupatia kamati pesa zikiongozwa na kamati ya Mheshimiwa Gitahi.

Mheshimiwa Kamala ameongea kama Mwinjilisti, karibu niulize wimbo wa maombi ni wa saa ngapi. Amekusifu kabisa na ninaona ya kwamba mambo yanaendelea vizuri. Asante na tupitishe huu mjadala kwa sababu ni wetu. Mvua ni baraka lakini akili nzuri ni baraka zaidi.

**Speaker:** Thank you, Hon. Members for a robust debate on a very timely motion.

*(Question put and agreed to)*

## ADJOURNMENT

**Speaker:** The sittings of this House now stand adjourned until next week Tuesday, 5th September, 2023 at 2.30 p.m.

The House rose at 3.10 p.m.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*